# Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

Toleo la 140 | Oktoba 2025


## Shime: Ewe mfugaji, hakikisha wanyama wako wanapata chanjo hii kutoka serikalini




***Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha sekta ya mifugo inachangia ipasavyo katika uchumi wa taifa. Mojawapo ya hatua hizo ni kupitia kampeni kubwa ya kitaifa ya uchanjaji wa mifugo, inayolenga kupunguza athari za magonjwa sugu yanayoshambulia mifugo nchini.***

---

Kwa muda mrefu, magonjwa ya mifugo yamekuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya sekta hii. Yamepunguza tija kwa wafugaji, kuathiri uzalishaji wa mazao ya mifugo, na kudhoofisha ushindani wa bidhaa za mifugo katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kutambua changamoto hii, serikali imechukua hatua za makusudi kwa kuanzisha mpango wa utoaji wa chanjo kwa wanyama kote nchini.

Serikali imetambua magonjwa hatari kama vile homa ya mapafu kwa ng'ombe, sotoka kwa mbuzi na kondoo, pamoja na magonjwa ya kuku kama kideri na ndui. Kupitia kampeni hii, serikali imeamua kugharamia sehemu kubwa ya chanjo hizo ili kuhakikisha wafugaji wanapata huduma hii kwa gharama nafuu. Kwa ng'ombe, mfugaji atalipia shilingi 500 tu kwa kila mnyama; kwa mbuzi na kondoo, shilingi 300; huku chanjo kwa kuku ikitolewa bure kabisa.

Kampeni hii ya kitaifa ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 16 Juni 2025, ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali kuboresha afya ya mifugo na kuinua kipato cha wafugaji. Wafugaji wote wanahimizwa kushirikiana na wataalamu wa mifugo katika maeneo yao kuhakikisha wanyama wote wanapata chanjo hizi kwa wakati, kwani zoezi hili linatarajiwa kufikia ukingoni mwezi Novemba mwaka huu.

***Ni wajibu wa kila mfugaji kuchangamkia fursa hii adhimu. Chanjo ni kinga, na kinga ni msingi wa mifugo yenye afya, tija na faida.***

### Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Fanya kilimo bila kemikali | 2 |
| Kilimo ikolojia ni suluhishio | 6 |





| | |
|---|---|
| Usitifue ardhi, funika udongo | 9 |
| Homa ya mapafu ya ng'ombe | 11 |


## *Mpendwa Mkulima*

*Kwa miaka mingi nchini Tanzania, na katika baadhi ya nchi za Mashariki mwa Afrika, shughuli za kilimo na ufugaji zimekuwa zikichukuliwa kuwa ni kazi za watu waishio vijijini, wazee, au wale wasio na uwezo wa kupata ajira rasmi. Vijana wengi wamekimbilia mijini wakitafuta kazi za maofisini au kujiingiza kwenye biashara, wakiamini kuwa huko ndiko kuna mafanikio. Hali hii imesababisha kushuka kwa uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara, na hivyo kuchochea ongezeko la bei sokoni kutokana na uhaba wa bidhaa hizo.*

*Matokeo yake ni kuyumba kwa uchumi wa maeneo ya vijijini na mijini, huku watu wa kipato cha chini wakikosa lishe bora na kuendelea kuishi maisha ya dhiki. Sekta ya kilimo na ufugaji, ingawa ni mhimili wa uchumi wa taifa, haikupewa kipaumbele stahiki. Vijana waliokimbilia mijini kwa matumaini ya ajira walijikuta wakikosa fursa, na hapo ndipo usemi usemao "shida ni mwalimu mzuri" ulipochukua nafasi yake.*

*Leo hii, wimbi la vijana wanaorejea vijijini na kujiingiza kwenye kilimo na ufugaji limekuwa likiongezeka kwa kasi. Wamegundua kuwa sekta hii ina ajira ya uhakika, kipato endelevu, na nafasi pana ya kujiajiri. Tumeshuhudia vijana wakianzisha mashamba ya kisasa, miradi ya ufugaji wa kisayansi, na hata kujiunga na vikundi vya wakulima ili kujifunza mbinu bora za uzalishaji.*

*Tunawapongeza vijana wote waliotambua kuwa kilimo na ufugaji si kazi ya dhiki, bali ni ajira ya heshima na msingi wa maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Kwa wale ambao bado hawajaanza, tunawatia moyo. Kumbuka, jembe halimtupi mkulima. Kilimo ni hazina, na ufugaji ni msingi wa uhakika wa chakula na kipato.*


+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu
mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org



Wasiliana na *MkM*,
S. L. P 14402, Arusha,
Simu: 0717 266 007, 0762 333 876,
Barua pepe:
info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

# Unaweza kufanya kilimo bila kutumia kemikali sumu yeyote

***Hivi ulishawahi kujiuliza kama unaweza kuzalisha mbogamboga, nafaka au matunda bila kutumia kemikali sumu yeyote kama vile mbolea pamoja na madawa na ukazalisha kwa wingi na kwa faida kubwa?***

**Digna Masawe**

Ukweli ni kwamba, uzalishaji wa chakula bila matumizi ya kemikali sumu yoyote unawezekana. Kwanza, kama utaangalia kwa umakini kuhusu afya yako na jamii ya watu wanaokuzunguka, mazingira, wanyama, mimea na udongo, kamwe hautafikiri kutumia kemikali sumu katika uzalishaji.

Mara nyingi wakulima na wafugaji wanaamini kuwa kwa kutumia dawa za viwandani zenye kemikali sumu, ndiyo uzalishaji wa kisasa. Dhana hii ni potofu, tena ni kujitengenezea kitanzi bila kujua. Ni dhahiri kuwa mnyororo wa madhara yanayotokana na matumizi ya kemikali sumu za viwandani na mbolea zisizokuwa za asili ni mrefu mno na madhara yake ni makubwa na yasiyoisha kirahisi.

Yapo muhimu yanayoweza kuzingatiwa kuhakikisha uzalishaji wa chakula salama na ndipo tunapozungumzia uzalishaji kwa misingi ya kilimo hai.

Kilimo hai kinaanzia kwenye utunzaji wa udongo. Huwezi kuwa na kilimo hai bila kuwa na udongo imara wenye rutuba. Pamoja na utunzaji wa udongo, pia ni muhimu sana kuzingatia utunzaji wa mazingira. Ni vigumu sana kufanya kilimo hai bila kufuata taratibu na kanuni sahihi zinazohitajika katika kutunza mazingira yanayokuzunguka na hata pengine popote utakapokuwa.

Kuna mambo kadhaa yanayobainishwa kuwa kama ni nyenzo ya uzalishaji wa chakula salama:

- Ni muhimu kufanya uhifadhi wa udongo, kwani kwa kufanya hivyo ni dhahiri kuwa utahifadhi rutuba na kuzalisha mazao yenye tija.
- Kuimarisha rutuba ya udongo huo kwa kutumia mbolea za asili kama vile mboji, samadi iliyoiva, mbolea ya minyoo (*vermicompost*), na mbolea ya kijani.
- Kuhakikisha unahifadhi rutuba hiyo ya udongo kwa njia za asili ili isipotee. Hii inaweza kuwa kwa kulima au kuotesha mazao funikizi kama vile kanavali, ngwara, kunde, au viazi vitamu.
- Ni muhimu kufanya kilimo cha mzunguko. Usilime shamba lote kwa mazao ya aina moja kila msimu. Unapoacha baadhi ya sehemu kishja kulima kwa msimu mwingine, unapandisha rutuba katika eneo hilo na kupunguza hatari ya magonjwa na wadudu.
- Kufuga wanyama kama vile ng'ombe, kuku, mbuzi, sungura nk. ili uweze kupata mbolea ya kupeleka shambani kwako. Pia, samadi ya wanyama hawa husaidia kuboresha muundo wa udongo.
- Epuka kufanya uchomaji shambani ili uweze kuhifadhi masalia ya mazao ili kupata mbolea na matandazo pamoja na kutunza bioanuai.
- Chagua mazao yanayofaa kulimwa katika eneo lako au mazao ya kikanda kulingana na hali ya hewa, aina ya udongo, na upatikanaji wa maji.
- Fanya kilimo cha mesto yaani kulima mazao zaidi ya moja katika eneo moja, kwa mfano kulima mahindi na maharage, au nyanya na vitunguu.
- Usitumie dawa zenye kemikali sumu katika kutibu magonjwa na wadudu. Ni vyema ukatumia dawa za asili kama vile mchanganyiko wa pilipili, tangawizi, majani ya mwarobaini, majivu, na sabuni ya mche. Dawa hizi ni salama lakini pia zina gharama nafuu.
- Kamwe usitumie mbolea za chumvi kukuzia mazao. Unapotumia mbolea hizi unachoma na kuua virutubisho muhimu kwa ajili ya mazao, na baadaye unapata mazao hafifu na yasiyokuwa na uhai. Mbolea hizi pia huharibu viumbe hai wa udongo kama minyoo na bakteria wa manufaa.




Mpangilio wa shamba na mazao

Ni muhimu kuhakikisha kuwa shamba lako lina mpangilio thabiti. Mpangilio wa shamba utawezesha uzalishaji wa aina mbalimbali za mazao. Unapokuwa na mpangilio, inasaidia kuepuka wadudu wanaoweza kushambulia mazao. Hii ni kwa sababu unakuwa na nafasi ya kupanda mchanganyiko wa mazao mbalimbali hasa mazao ya mbogamboga. Hali hiyo inasaidia kuzuia uwepo wa wadudu na magonjwa. Pia, mpangilio mzuri husaidia katika usimamizi wa maji, mwanga, na hewa.

MUHIMU Kama tulivyoeleza hapo juu, ni vyema zaidi kama utafanya kilimo mesto, yaani kilimo cha mazao pamoja na wanyama. Hii itakusaidia kupata mbolea kwa ajili ya kulisha rutuba ya udongo lakini pia utapata chakula kutoka shambani na kwa wanyama, hivyo utaweza kupata makundi yote yanayotakiwa mwilini kupitia shamba lako. Zaidi ya hayo, kilimo mseto huongeza kipato, hupunguza hatari ya hasara, na huongeza uthabiti wa mfumo wa uzalishaji.

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

**Mpangilio**: Cathbert Msemo 0757 847 481
**Mhariri:** Erica Rugabandana
**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni
**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876
Barua pepe: info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org





# Fahamu namna sahihi ya kuwakinga kuku wako na magonjwa

***Kwa muda mrefu sana, wafugaji wengi wa kuku wamekuwa wakikumbana na changamoto za wadudu pamoja na magonjwa yanayoshambulia kuku. Hali hii imekuwa ikisababisha hasara kubwa inayowakatisha tamaa wafugaji.***

**Eliudi Letungaa**




Katika kuelekea mvua za vuli, tungependa wafugaji wa kuku wafahamu baadhi ya magonjwa na namna ya kukabiliana nayo pamoja na wadudu wanaoshambulia kuku—jambo litakalowawezesha kuepukana na hasara na kuwa na miradi yenye tija.

Aidha, mfugaji atafahamu chanjo muhimu kwa kuku pamoja na ratiba yake ili kuweza kuwa na ufugaji wa kuku wenye tija. Ni muhimu kwa mfugaji kuhakikisha kuwa anafahamu na kuzingatia chanjo na ratiba kwa kuku wake.

Endapo mfugaji atashindwa kuwapatia kuku chanjo kwa kufuata ratiba sahihi, ni dhahiri kuwa atakuwa katika hatari kubwa ya kupoteza mifugo yake kwani hawataweza kustahimili magonjwa.

## Chanjo muhimu na kinga dhidi ya wadudu na magonjwa yanayoshambulia kuku

### Chanjo na ratiba maalumu

1. Siku ya 1 – Mara baada ya vifaranga kutotoleshwa, ndani ya siku moja wapewe glucose kwa muda wa masaa mawili. Glucose huchanganywa katika maji na kupewa vifaranga hawa. Baada ya hapo, wapewe mchanganyiko wa vitamini mfano Aminovit na OTC Plus, pia huchanganywa na maji. Vifaranga wawekwe katika eneo safi na lenye joto la wastani.
2. Siku ya 7 – Vifaranga wapatiwe chanjo ya Kideri (Newcastle). Chanjo huchanganywa na maji safi katika eneo lenye kivuli, kisha kupewa vifaranga kwa muda wa masaa mawili. Baada ya hapo, maji hayo yamwagwe mbali na eneo la kuku wengine au yachimbwe. Kisha wapewe maji yenye mchanganyiko wa vitamini.
3. Siku ya 14 – Vifaranga wapewe chanjo ya Gumboro (IBD). Chanjo huchanganywa katika maji na kupewa vifaranga kwa muda wa masaa mawili tu. Baada ya hapo, wapewe mchanganyiko wa vitamini. Kuku waliokufa kwa ugonjwa huu hutambulika kwa kuchana vifua vyao na kuona vidoti vyekundu.
4. Siku ya 21 (Wiki ya 3) – Rudia chanjo ya Kideri (Newcastle).
5. Siku ya 28 (Mwezi) – Rudia chanjo ya Gumboro (IBD).
6. Siku ya 35 (Mwezi 1 na Wiki 1) – Wapewe mchanganyiko wa vitamini ya kutosha.
7. Wiki ya 6–8 – Wapewe kinga ya Ndui (Fowl Pox). Kinga hii si rahisi kwa mfugaji asiye na utaalamu, hivyo tafuta mtaalamu wa mifugo au maelekezo sahihi ya jinsi ya kuweka kinga hii.
8. Wiki ya 8 – Wapewe dawa ya minyoo kama Piperazine. Baada ya hapo, unaweza kurudia chanjo ya Newcastle.




### Namna sahihi ya kudhibiti magonjwa ya kuku

- Tunza hali ya usafi ndani ya banda na udhibiti unyevu.
- Badili matandazo yanapochafuka.
- Vyombo vya maji visafishwe kila siku.
- Epuka kufuga kwa njia huria ili kuku wasiambukizwe magonjwa kwa urahisi.
- Epuka kufuga kuku pamoja na bata na kanga, hawa ni wabebaji wa vimelea vya magonjwa japo wao hubaki salama.

### Mambo ya kujiepusha nayo katika ufugaji wa kuku

Ni ukweli usiopingika kuwa katika ufugaji kuna baadhi ya mambo wafugaji hufanya, lakini hayakupaswa kufanyika. Yafuatayo ni mambo ya kujiepusha nayo:

- Epuka kuacha banda likiwa chafu bila chanzo cha nishati kama umeme, sola au jenereta.
- Epuka kutibu kwa mazoea bila kuwasiliana na Afisa Mifugo.
- Epuka kutembelea mabanda ya jirani bila kuchukua tahadhari.
- Epuka kuleta na kuingiza kuku wageni bila kujua historia ya chanjo walipotoka.
- Epuka kuuza kuku wagonjwa.
- Epuka kuchinja kuku wagonjwa.
- Epuka kununua kuku wagonjwa.
- Epuka kutupa kuku waliokufa porini.
- Zingatia ratiba za chanjo kwa magonjwa yasiyo na tiba kama Kideri na mengineyo ya virusi.
- Epuka kununua chanjo kutoka kwa wauzaji wasio na nishati sahihi ya kuhifadhi chanjo.

Katika ufugaji, jambo kubwa na muhimu ni kuzingatia usafi. Bila usafi, hata uwe unawapatia chakula cha aina gani, kuku hawawezi kufanya vizuri.

# Kutumia aloe vera (shubiri mwitu) na mpapai kutibu magonjwa ya kuku

***Magonjwa mengi ya kuku yanaweza kutibiwa kwa kutumia mimea tiba asilia na kuepukana na sumu za viwandani ambazo zina madhara kwa wanyama na kwa walaji. Moja ya mimea inayoweza kutumiwa kutibu magonjwa ya kuku ni aloe vera (shubiri mwitu) pamoja na mpapai.***

**Flora Laanyuni**


Picha:MkM



## 1. Shubiri mwitu

Kutumia Shubiri Mwitu Kusafisha Vidonda

### Namna ya kuandaa:

Chukua majani ya shubiri mwitu na uyachane vipande vidogo vidogo.

- Vitwange pamoja na pumba kidogo kisha uvianike.
- Vikisha kauka, vitwange tena na uchekeche upate unga laini.
- Hifadhi unga katika chombo kisafi na kikavu.

### Namna ya kutumia:

- Safisha vidonda vilivyotokana na ndui au vidonda vyovyote kwa maji safi yenye chumvi kiasi.
- Pakaa unga wa shubiri mwitu katika vidonda vilivyosafishwa.
- Rudia baada ya siku moja. Endelea kutumia hadi vidonda vikauke.

Kudhibiti Magonjwa Mengine ya Kuku kwa Kutumia Shubiri Mwitu

### Maandalizi:

- Chukua jani moja la shubiri mwitu lenye ukubwa wa kati.
- Likate vipande vidogo vidogo.
- Loweka vipande hivyo katika maji kiasi cha lita mbili.

### Namna ya kutumia:

Kuku watumie maji haya kwa kunywa siku zote.

Hii husaidia kuwakinga dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Badilisha maji kabla hayajaanza kuchacha na tengeneza dawa mpya.

Hakikisha chombo kinasafishwa vizuri kabla ya kuweka dawa nyingine.

## 2. Mmea wa mpapai

Kutibu Kuharisha kwa Kuku

### Namna ya kuandaa:

Pata jani moja bichi la mpapai na uliponde ponde hadi lilainike.

Changanya na maji kiasi cha lita mbili na nusu.

### Namna ya kutumia kama tiba:

- Kuku wapewe maji hayo wanywe, wasipewe maji mengine kwa ajili ya kunywa kwa siku angalau nne au zaidi.
- Inafaa zaidi kuwaandalia dawa mpya kila siku ili isiharibike.

### Kutumia mpapai kupambana na magonjwa ya kuku

### Namna ya kutumia kama kinga:

- Hata kama kuku hawaharishi, wakizoeshwa kunywa maji yenye majani ya mpapai yaliyopondwa angalau mara tatu kwa wiki, watakingwa dhidi ya magonjwa mengi.

Njia Nyingine ya Kutumia Mpapai

### Namna ya kuandaa na kutumia:

Chukua majani ya mpapai uyatwange upate kisamvu chake kiasi cha lita moja.

### Changanya kisamvu hicho na pumba lita mbili.

Waweza kuongezea maji kidogo na kuwapatia kuku wanaoumwa watumie chakula hicho hadi wapone.

Kama kuku ni wachache, andaa chakula wanachoweza kumaliza kwa siku moja ili kisibakie na kuharibika kabla hawajakimaliza.

***Makala hii ni kwa hisani ya Rural Livelihood Development Company, www.rldc.co.tz / info@rldc.co.tz.***





# Siku ya chakula duniani – "Sayansi katika vitendo" kwa uzalishaji wa chakula salama kupitia kilimo ikolojia

***Kila tarehe 16 Oktoba, dunia huadhimisha Siku ya Chakula Duniani, ikiwa ni fursa ya kimataifa ya kuangazia changamoto na mafanikio katika sekta ya chakula na lishe. Mwaka huu, kauli mbiu ya maadhimisho ni "Sayansi katika Vitendo", ujumbe unaosisitiza umuhimu wa kutumia maarifa ya kisayansi kwa njia ya vitendo ili kuboresha mifumo ya chakula duniani.***

**Erica Rugabandana**


Picha:MkM

Katika muktadha huu, mfumo wa kilimo ikolojia umeibuka kuwa moja ya njia za kisayansi na endelevu za kuzalisha chakula salama, kulinda afya ya mlaji, na kuhifadhi mazingira.

### Sayansi katika vitendo: inamaanisha nini?

Kauli mbiu ya mwaka huu inalenga kuhamasisha utekelezaji wa suluhisho za kisayansi, si tu kwa nadharia, bali kwa vitendo vinavyoleta mabadiliko halisi kwa jamii. Hii ni pamoja na:

- Matumizi ya mbinu bora za kilimo
- Usindikaji salama wa chakula
- Uvumbuzi wa teknolojia rafiki kwa mazingira
- Maarifa ya kuimarisha lishe bora katika ngazi ya familia na jamii

### Changamoto ya chakula salama

Dunia inakabiliwa na changamoto kubwa za usalama wa chakula: ongezeko la watu, mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, na matumizi mabaya ya viuatilifu na kemikali katika kilimo. Watu wengi wanaathirika kiafya kutokana na kula chakula chenye mabaki ya sumu, ambacho huzalishwa bila kuzingatia usalama wa mlaji.


Picha:IN

Ni wazi sasa kwamba suluhisho la kudumu linahitaji matumizi ya sayansi katika njia ambazo ni rafiki kwa afya na mazingira. Hapa ndipo kilimo ikolojia kinapoingia kama jibu muhimu.

### Kilimo ikolojia: Sayansi ya asili kwa chakula salama

Kilimo ikolojia ni mfumo wa kilimo unaotegemea kanuni za kisayansi zinazozingatia uhusiano wa viumbe hai na mazingira yao. Unahusisha mbinu kama:

- Kutumia mbolea za asili kama mboji na samadi
- Kupanda mazao mseto kwa kuzuia magonjwa na kulinda udongo
- Kutumia mimea na wadudu rafiki kuzuia wadudu waharibifu (biological pest control)
- Kuhifadhi maji na rutuba ya udongo kwa kutumia matandazo na kilimo cha mzunguko

Hizi zote ni mbinu za kisayansi zinazowekwa katika vitendo na wakulima, hasa wadogo, ili kuzalisha chakula salama na chenye virutubisho vya kutosha.

### Faida za kilimo ikolojia kwa chakula salama

Chakula Kisicho na Kemikali Hatari Mazao ya kilimo ikolojia hayana mabaki ya viuatilifu au mbolea za viwandani ambazo huweza kusababisha magonjwa ya muda mrefu kama saratani na matatizo ya uzazi.

Lishe Bora kwa Mlaji Udongo wenye afya huzalisha chakula chenye virutubisho vingi, na hivyo kuchangia mwili wenye kinga imara dhidi ya maradhi.

Mazingira Salama Kwa kutotumia kemikali, kilimo ikolojia huchangia kupunguza uchafuzi wa maji, hewa na udongo, jambo linaloendana kikamilifu na lengo la sayansi endelevu.

Uimara wa Wakulima Wadogo Mbinu hizi huwawezesha wakulima kuzalisha kwa gharama ndogo, kwa kutumia rasilimali walizonazo, huku wakihifadhi mazingira yao kwa vizazi vijavyo.

### Hitimisho

Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani mwaka huu yanatufundisha kwamba sayansi haitakiwi kubaki kwenye vitabu au maabara pekee, bali kutumika kwa vitendo kusaidia jamii zetu. Kilimo ikolojia ni mfano hai wa jinsi sayansi ya mazingira, lishe, na kilimo inavyoweza kutumika kwa vitendo kuzalisha chakula salama, kulinda afya, na kuhifadhi mazingira.

Katika safari ya kuelekea mifumo bora ya chakula duniani, ni muhimu kutambua kuwa chakula salama si anasa, ni haki ya binadamu. Na kilimo ikolojia ni moja ya njia bora kabisa za kuhakikisha haki hiyo inatimizwa kwa wote.

# Kilimo-ikolojia: Suluhisho la mabadiliko ya tabianchi

***Miongoni mwa mbinu zinazopendekezwa za kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, kilimo-ikolojia kinajitokeza kama njia madhubuti, endelevu na yenye kustahimili misukosuko. Mbinu hii hutoa suluhu zinazojikita katika uhusiano wa moja kwa moja kati ya binadamu na mazingira, huku ikihakikisha usalama wa chakula na kulinda ikolojia kwa vizazi vya sasa na vijavyo.***

**Magreth Mollel**

Kilimo ikolojia ni mfumo wa kilimo unaozingatia afya ya mimea, wanyama, mazingira na lishe bora. Mfumo huu wa kilimo unahakikisha mazingira yanakuwa endelevu na salama, kama vile udongo, maji na hewa, vile vile kuhakikisha uzalishaji wa chakula salama kwa afya ya binadamu na viumbe wengine bila kutumia bidhaa zozote hatarishi kama mbolea za viwandani na viuatilifu vyenye sumu.

Katika vipengele vifuatavyo, tutaangazia namna kilimo ikolojia ni mfumo salama na suluhisho la kina katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi:

## i. Matumizi ya rasilimali asilia

Kilimo ikolojia kinawapa wakulima nafasi ya kutumia rasilimali zilizopo kama mbolea ya asili (mboji, samadi, majani yaliyooza), mbegu za kienyeji, na maarifa ya jadi kupunguza utegemezi wa pembejeo za kibiashara zenye gharama kubwa. Kwa mfano, wakulima wa maeneo ya vijijini wanapotumia samadi badala ya mbolea ya viwandani, wanapunguza gharama na kulinda afya ya udongo.



Picha:MkM



Picha:MkM

Mbinu hizi huongeza uwezo wa mashamba kustahimili mshtuko wa tabianchi kama vile ukame, mvua zisizotabirika, na mabadiliko ya msimu. Mashamba yanakuwa na uwezo wa kuhimili hali ngumu bila kutegemea soko pekee, bali kwa kutumia rasilimali walizonazo na maarifa ya ndani ya jamii. Aidha, matumizi ya mbegu za kienyeji huongeza uwezo wa mazao kuhimili magonjwa na hali ngumu ya hewa, kwani mbegu hizo zimezoea mazingira husika kwa muda mrefu. Hii huongeza uhakika wa mavuno na kupunguza hatari ya hasara kwa wakulima wadogo.

## ii. Matumizi ya maarifa ya kienyeji na sayansi

Mbinu za kilimo ikolojia zinachanganya maarifa ya asili ya wakulima na uvumbuzi wa kisayansi. Kwa mfano, wakulima katika Kanda ya Kaskazini mwa Tanzania wamekuwa wakitumia mzunguko wa mazao na mazao mchanganyiko kwa vizazi vingi, mbinu inayosaidia kupunguza magonjwa ya mimea, kudhibiti wadudu, na kuimarisha rutuba ya udongo.

Utafiti wa kisasa kutoka taasisi kama *ICRAF, Sokoine University of Agriculture, na Bioversity International* unathibitisha kuwa mbinu hizi zina mchango mkubwa katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Sayansi inathibitisha kile ambacho wakulima wa jadi wamekuwa wakifanya kwa ufanisi kwa miaka mingi. Ushirikiano kati ya watafiti na wakulima unazidi kuimarisha mbinu hizi, na kuzifanya ziweze kutumika kwa ufanisi zaidi katika maeneo mbalimbali. Hii huongeza imani ya jamii katika maarifa yao ya jadi na kuchochea ubunifu wa ndani.

## iii. Ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali asilia

Kupitia mbinu za kuhifadhi udongo na maji, misitu-shambani (*agroforestry*), na matumizi ya matandazo, kilimo-ikolojia huzuia mmomonyoko wa ardhi, huhifadhi unyevu, na huboresha afya ya udongo. Kwa mfano, wakulima wanaotumia matandazo ya majani au mabaki ya mazao huongeza unyevu wa udongo na kupunguza joto kali ardhini.

Mbinu hizi pia husaidia kudhibiti magugu, kupunguza matumizi ya nguvu kazi, na kuongeza viumbe hai wa udongo kama minyoo na bakteria wa manufaa. Kwa kutumia miti ya kivuli na ya matunda katika mashamba, wakulima huongeza bioanuai, kupunguza joto, na kuboresha muundo wa udongo. Hii inasaidia kupunguza athari za ukame, kuimarisha ustawi wa mazao katika misimu ya mvua hafifu, na kuongeza uzalishaji hata katika maeneo yenye changamoto za hali ya hewa. Zaidi ya hayo, matumizi ya matandazo husaidia kuhifadhi virutubisho vya udongo na kupunguza uharibifu wa tabaka la juu la ardhi.

## iv. Kupunguza uzalishaji wa gesi jotozi

Tofauti na kilimo cha kisasa kinachotegemea mbolea za kemikali na mashamba makubwa yanayochochea ukataji wa miti, kilimo-ikolojia hupunguza uzalishaji wa gesi zinazochangia ongezeko la joto duniani kama methane na *nitrous oxide*.

Kupitia kupanda miti shambani, kutumia mbolea za asili, na kurejesha hekta zilizoharibika kwa njia ya kilimo cha kurejesha ardhi (*regenerative agriculture*), wakulima wadogo huchangia moja kwa moja juhudi za kupunguza mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kwa kuepuka uchomaji wa mashamba na badala yake kutumia masalia ya mazao kama matandazo, wakulima hupunguza uzalishaji wa kaboni na kulinda tabaka la juu la udongo. Hii ni hatua ya kisayansi na kijamii inayoweza kuleta mabadiliko makubwa duniani. Kwa kuzingatia mbinu hizi, wakulima wanakuwa sehemu ya suluhisho la kimataifa dhidi ya ongezeko la joto duniani.

## v. Kuongeza usalama wa chakula

Kilimo ikolojia kinahimiza utofauti wa mazao shambani. Kwa mfano, wakulima wanapochanganya mahindi, kunde, mboga, na matunda, wanapata lishe bora kwa familia zao na pia hupunguza hatari ya kukosa chakula wakati mazao fulani yanaposhindwa.

Utofauti huu wa mazao huongeza kinga ya jamii dhidi ya njaa, huimarisha afya ya walaji, na huongeza mapato kwa kuuza mazao mbalimbali sokoni. Pia husaidia kupunguza utegemezi wa mazao ya kibiashara pekee kama mahindi au mpunga. Kwa kuongeza mazao ya thamani kama mboga mboga, matunda, na viungo, wakulima huongeza kipato na kuboresha lishe ya familia zao. Hii ni hatua muhimu katika kupambana na utapiamlo na umasikini wa kipato. Aidha, wakulima wanapojifunza kuhifadhi mazao yao kwa njia za asili, huongeza muda wa matumizi na kupunguza upotevu wa chakula.

## vi. Kuwezesha ushirikiano na nguvu za jamii

Mbinu za kilimo ikolojia mara nyingi hutekelezwa kupitia ushirikiano wa kijamii: vikundi vya akiba, mabenki ya mbegu, shule za mashamba, na mashirika ya kijamii. Ushirikiano huu unawawezesha wakulima wadogo kubadilishana mbegu, maarifa, uzoefu, na hata msaada wa kifedha.



Picha:MkM

Kwa mfano, vikundi vya wakulima wa wanawake katika Mkoa wa Morogoro wamefanikiwa kuanzisha mashamba ya pamoja ya kilimo ikolojia, na sasa wanauza mazao ya mboga mboga salama kwa shule na hospitali. Ushirikiano huu hujenga mtandao wa pamoja wa kustahimili mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uchumi wa jamii. Pia huongeza ushawishi wa wakulima katika kupanga sera za kilimo, kuomba rasilimali, na kushiriki katika mafunzo ya kitaalamu. Ushirikiano huu huimarisha mshikamano wa kijamii na kuchochea maendeleo ya pamoja.

## Hitimisho

Kilimo ikolojia siyo tu mbinu ya kilimo, bali ni mfumo wa kijamii na kiikolojia unaotoa suluhu za kina kwa changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Ni njia ya kisayansi inayojumuisha maarifa ya jadi, uvumbuzi wa kisasa, na mshikamano wa kijamii.

Kupitia kilimo ikolojia, wakulima wadogo wa Tanzania wanaweza kulima kwa kuendana na mazingira, kujenga ustahimilivu, na kuhakikisha usalama wa chakula kwa jamii zao. Ni wakati wa kuwekeza katika maarifa haya, kuyahamasisha, na kuyatumia kama nguzo ya maendeleo ya kilimo na ustawi wa jamii. Serikali, mashirika ya kiraia, taasisi za utafiti, na sekta binafsi wanapaswa kushirikiana kuendeleza kilimo-ikolojia kama msingi wa sera za kilimo na mabadiliko ya tabianchi. Hii ni fursa ya kipekee ya kujenga mifumo ya chakula inayostahimili misukosuko ya hali ya hewa, inayolinda mazingira, na inayowezesha jamii kujitegemea kiuchumi na kiafya.

Kwa kuwekeza katika kilimo-ikolojia, tunaweka msingi wa maendeleo jumuishi, yanayozingatia utu, haki ya chakula, na hifadhi ya mazingira. Ni wakati wa kuhamasisha sera zinazounga mkono wakulima wadogo, kuimarisha tafiti za kilimo endelevu, na kuunda mifumo ya masoko inayotambua thamani ya mazao salama na ya ikolojia.

***Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Magreth Mollel, Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa simu namba 0756529127.***

# Je, Una swali lolote kuhusiana na ufugaji wa samaki? Tuulize nasi tukujibu

***Ni utaratibu wa kawaida kabisa kwa MkM kuthamini maoni yako na kujibu maswali yenu kupitia wataalamu wa kada mbalimbali. Katika toleo hili, Musa Said ambaye ni mtaalamu wa samaki anaendelea kujibu maswali kuhusiana na ufugaji wa samaki. Hivyo, kama nawe una maswali basi usisite kutuuliza ili upate jibu.***

**Irene Mark**

***Lai Otieno anauliza: Mimi natoka Musoma mjini na nataka kufuga samaki kwa njia ya kisasa. Je, bwawa naweza kuweka mbali na maeneo ya ziwa au jirani na ziwa? Pili, kuna uwezekano wa kutumia maji ya bomba?***

**Musa Said anajibu:** Itakuwa vizuri ukiweka umbali usiopungua mita 10 kutoka ziwani. Inawezekana pia kutumia maji ya bomba, cha msingi hakikisha yasiwe na kemikali. Ingawa ni vizuri zaidi maji hayo yakiwa yamepimwa na wataalamu. Ahsante.

***Robert Kidemi: Mimi nimeshaanza kuweka mtaji kwa ajili ya kufuga samaki, ninataka kujua kuhusu maji sahihi ya kufugia na uandaaji wa bwawa la samaki.***

**Musa Said anajibu:** Ufugaji wa samaki kama ilivyo shughuli nyingine yoyote ya kiuchumi, unahitaji usimamizi mzuri ili uweze kuwa na faida. Mbali na hilo, mfugaji wa samaki anatakiwa kuzingatia vigezo vingi kabla ya kuanza ufugaji. Moja ya vigezo muhimu vya kwanza ni soko. Si jambo la busara kuanza shughuli yoyote kabla haujafanya uchunguzi na kujua kama kuna mahitaji ya bidhaa unayokusudia kuzalisha. Wafugaji wengi wameanzisha ufugaji




wa samaki lakini wakaishia kupata hasara kutokana na ukosefu wa soko. Na wengine wameanguka kutokana na utunzaji mbovu wa mabwawa ya samaki.

Kuhusu suala la maji, upatikanaji wa maji na ubora wake ni kigezo muhimu katika ufugaji wa samaki. Mtiririko wa maji ni njia rahisi kwa mfugaji. Maji machafu hayatakiwi kwa ufugaji wa samaki. Wafugaji ni lazima wasaidiwe na maafisa kilimo katika eneo lao ili kujua kama maji yanayopatikana yana ubora kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Maji kutoka vyanzo vyovyote yanaweza kufaa kufugia, lakini ni lazima kwanza yapimwe kujua kama ni salama na hayana kemikali yeyote ya kuweza kudhuru samaki wako.

Kuhusu bwawa; hili linahitaji nafasi kubwa ya ardhi, yenye mwinuko pamoja na eneo la samaki kukimbilia. Hii ni njia rahisi ya ufugaji endapo ardhi na maji havina gharama kubwa. Eneo kubwa zaidi linaruhusu uzalishaji usiohitaji nguvu ya ziada na wenye tija.

Utengenezaji wa bwawa la samaki kwa maeneo yenye udongo wa kichanga, mfugaji atalazimika kuchimba na kuweka karatasi ya nailoni. Hii itasaidia kuzuia upotevu wa maji pamoja na kuzuia bwawa kuporomoka.

Ni vyema upande mmoja wa bwawa ukawa na kina kirefu kuliko mwingine cha mita moja na nusu, na mwingine mita moja. Hii itamsaidia mfugaji kuweza kulihudumia bwawa vizuri, hata kama ni kuingia na kufanya usafi.

***Jonathan anauliza: Mimi nakaa Kigamboni maeneo ya Mwembe Mdogo na eneo langu lina udongo wa mfinyanzi sehemu kubwa na maji yapo karibu sana. Ukichimba nusu mita unakutana na maji mengi. Pia nina kisima cha kupandisha na mota cha mita 50, maji yake ni baridi (hayana chumvi hata kidogo na ni mengi). Je, uchimbaji wa bwawa la samaki unahitaji kusakafia kwa sementi? Je, makadirio ya uchimbaji bwawa sehemu kama hii inaweza kugharimu kiasi gani kitaalamu? Pia, samaki aina ya sato dume anauzwaje kwa kifaranga (huko juu ulisema kwa pelege, au pelege ndo sato?). Pia ulisema, ufugaji wa semi-extensive unaanzia samaki wa 4–10 kwa square mita moja. Je, kwa sato dume unaweza kufuga samaki 10 kwa square mita moja? Nikitaka kufanya ufugaji huu kuwa ndiyo biashara yangu ya uzalishaji, je, unaweza kunipa mchanganuo na faida yake, kwa mfano ukianza na samaki 2000?***

**Musa Said anajibu:** Uchimbaji wa bwawa la kufugia samaki si lazima lijengewe kwa simenti. Kikubwa sana tunachokizingatia ni uthibiti wa maji ndani ya bwawa usipungue chini ya mita moja au moja na nusu. Na hii ni kulingana na tabia ya eneo lako la mradi likoje na linahitaji bwawa la aina ipi.

Gharama za uchimbaji kwa kweli hazipo maalumu kulingana na sehemu husika. Mara nyingi tunakupigia gharama baada ya kuona eneo lako lipoje na pia mradi wako unataka uwe wa ukubwa gani, na mambo mengine mengi ambayo tutayadadisi kwenye eneo lako na baadaye kukupa gharama halisi ya kitaalamu.

Gharama ya sato dume ni Tsh 200 tu. Kuweka samaki 10 kwa mita moja ya mraba inawezekana, lakini lazima mtaalamu awe karibu sana. Uwekaji kwa wingi ndani ya bwawa unahitaji umakini na uelewa wa hali ya kumtambua samaki anataka nini, kwanini, kwa wakati gani, na ufanye nini.








# Usitifue ardhi; penda kufunika udongo kila msimu wa kilimo

***Ni kwa namna gani udongo unaweza kufunikwa wakati wote, na shughuli nyingine za kilimo zikawa zinaendelea? Hili ni swali muhimu wanalojiuliza wakulima wengi.***

**Flora Laanyuni**

Hii inategemeana na utunzaji na aina ya shughuli zinazofanyika kwenye udongo huo, na kama shughuli zenyewe zinafanyika kwa kutumia mikono au mashine. Moja ya shughuli ambazo zinasumbua udongo kwa kiasi kikubwa ni kulima kwa kutumia jembe la kukokota kwa ng'ombe au trekta.

Tunaposema kufunika udongo, uelewa wa sababu ya kufunika udongo ni muhimu sana.

Baada ya kufanya mambo yote, tunafunika udongo ili kuzuia mmomonyoko, virutubisho kutoweka, kukauka, kupasuka na mengineyo.

## Hili linaweza kufanyika kwa njia mbalimbali:

1. Kwa kutumia mimea inayotambaa, ambayo mara nyingi huwa tunaipanda.
2. Kwa kutumia matandazo, ambayo yanaweza kuwekwa chini ya shina la mimea au kutandazwa kwenye ardhi ambayo bado haijalimwa.
3. Kuweka kivuli kwa kutumia turubai.
4. Kivuli cha miti.

Kila njia inatofautiana kulingana na mahitaji na uwezo wa mkulima.

Katika hali kama hii, mkulima anaweza kuacha kabisa kutifua udongo, ambapo katika sehemu kama hiyo udongo ubaki ukiwa umefunikwa siku zote kutokana na mabaki ya mazao yaliyovunwa kabla ya kupanda mengine.

## Kulima kwa jembe la kukokotwa na wanyama

Sehemu ambayo ardhi imelimwa




kwa kutumia plau, matandazo huondolewa au kusogezwa.

Hata hivyo, inapendekezwa kufunika udongo mara moja, ili kuepusha mmomonyoko, au upotevu wa virutubisho pamoja na udongo kukauka. Wakulima walio wengi katika nchi zinazoendelea wanageukia kulima sehemu ambayo ilikuwa haitifuliwi, ambapo wanatumia trekta, plau na hata kupanda kwa kutumia harrow.

Hii inasemekana kuwa inarahisisha kazi ikiwa ni pamoja na kupata mavuno mengi, lakini si kweli kwani ardhi isiyolimwa/tifuliwa hupunguza gharama, hulinda udongo, pamoja na kuongeza mavuno.

## Ardhi isiyolimwa au kutifuliwa

Aidha, kutokana na kufunikwa kwa udongo, magugu huzuiliwa kuota na hupelekea kupunguza gharama za kupalilia. Rutuba ya udongo huongezeka, hivyo kuwa na mazao yenye afya. Viumbe hai kwenye udongo huongezeka na hivyo kujenga muundo mzuri zaidi wa tabaka za udongo, ambao una uwezo wa kukabiliana kwa kiasi kikubwa na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi.




## Punguza kuutifua udongo, zuia magugu

Kila gramu moja ya udongo ina mamilioni ya mbegu za magugu. Ili mbegu iote, inahitaji kupata mwanga na jua. Kulima hupelekea kugeuza mbegu zilizokuwa zimefukiwa kwenye udongo kuwa juu na hivyo kuzifanya ziote. Hivyo, kutifua udongo husaidia kuongeza magugu shambani.

Kwa upande mwingine, kuweka matandazo shambani husaidia kuzuia mwanga kufikia ardhi, hivyo kuzuia magugu kuota. Kuacha kulima huku ukifunika udongo kwa matandazo husaidia kuzuia magugu, hivyo kuondoa gharama ya muda na nguvu kazi ya kufanya palizi, na kuwa na udongo wenye afya.

## Kulima huharibu viumbe hai waliomo kwenye udongo

Kutifua ardhi huharibu baiyoanuai yaani viumbe hai wadogo waliopo kwenye udongo ambao wana faida kwa ufanisi wa udongo. Aina tofauti ya viumbe hai muhimu huishi katika matabaka tofauti ya udongo. Tunapotifua udongo, si tu kuwa tunaweka mbegu za magugu juu na kuzifanya ziote, lakini pia tunaharibu hali ya viumbe hai walio muhimu kwenye udongo.

Matokeo yake ni kuwa udongo utahitaji kuboreshwa kabla ya kurudi kwenye hali yake ya kawaida. Udongo uliokauka unaweza kuhitaji kutifuliwa kidogo ili kuruhusu hewa kuingia, lakini hatua hii pia inaweza kuachiwa viumbe hai wadogo kwenye udongo kuifanya.

Kunyunyizia kemikali kwenye mimea huua wadudu muhimu kwenye udongo na hivyo kusababisha gharama isiyohitajika kwa mkulima. Mkulima mzuri hujenga mazingira mazuri ya hawa wadudu kuendelea kuwepo kwenye udongo.

# Ni muhimu kufahamu magonjwa ya ng'ombe na namna ya kukinga ili kuepuka hasara za vifo

***Mimi ni msomaji wa jarida la MkM, napenda kuanzisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ila nimekuwa nikitatizwa na hofu ya magonjwa. Je, naweza kufahamu baadhi ya magonjwa yanayoshambulia ng'ombe mara kwa mara ili niweze kujifunza namna ya kukabiliana nayo?***

**Linus Prosper**

Kuna magonjwa mengi sana yanayoshambulia ng'ombe na kusababisha madhara kiuchumi na kwa maendeleo ya sekta ya mifugo.

Pamoja na hayo, magonjwa mengi ya ng'ombe yanatibika kwa haraka endapo mfugaji atawahi. Katika makala hii tutaainisha baadhi ya magonjwa muhimu yanayoshambulia ng'ombe mara kwa mara katika kanda mbalimbali.

## 1. Ugonjwa wa kimeta

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria ambao huishi ardhini kwa miaka mingi. Bakteria hawa huingia mwilini mwa ng'ombe kupitia jeraha la puani na mdomoni.

### Dalili za ugonjwa:

- Ni vigumu kuona au kutambua dalili kwa kuwa ugonjwa huua mnyama ghafla sana.
- Dalili kubwa ni wanyama wengi kufa ndani ya siku mbili tu bila kuumwa.
- Damu hutoka katika midomo, masikio, pua, ikiwa na rangi nyeusi ambayo haigandi.

**Angalizo:** Mfugaji asithubutu kugusa nyama ya ng'ombe aliyekufa, kwani haifai kwa matumizi ya binadamu.

### Kuzuia kimeta:

- Kuchoma na kufukia mizoga yote ya ng'ombe aliyekufa.
- Udongo, nyasi za kulalia, tandaza chokaa juu ya shimo la futi 6.
- Chanja wanyama wote wazima kwa dawa inayopendekezwa na wataalamu.
- Wanyama wenye umri wa zaidi ya miezi sita wapatiwe chanjo kila mwaka kwa muda wa miaka 3 tangu mlipuko utokee.

**Tiba ya Kimeta:** Wanyama watibiwe kwa kutumia dawa ya penicillin na daktari wa wanyama/mifugo.




## 2. Tatizo la mimba kuharibika

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria ambaye hupenyeza hadi kwenye tumbo la uzazi na kuachanisha kichanga na ng'ombe, hivyo kusababisha mimba kutoka katika kipindi cha miezi 4–7.

Bakteria hao husababisha kutoka mimba kwa ng'ombe, pamoja na nguruwe na mbuzi.

### Dalili za ugonjwa:

- Uvimbe kwenye tumbo la uzazi na mafua ya uzazi.
- Kutoka mimba yenye umri wa miezi 5–8.
- Ng'ombe hushindwa kushika mimba.

### Tiba:

- Hakuna tiba muafaka ya ugonjwa.
- Tiba inayotumika ni kuchinja wanyama walioathirika.
- Tenganisha wanyama waliotoka mimba na wazima kwa muda wa wiki 3.
- Chanja ndama wa miezi 3–9 mara kwa mara.
- Choma masalia ya vifaa vilivyoathirika.

## 3. Ugonjwa wa miguu na midomo

Ugonjwa huu husababishwa na virusi. Hasara kubwa ya ugonjwa huu ni kupungua kwa uzalishaji wa maziwa kutokana na vifo.

### Dalili za ugonjwa:

- Ng'ombe hudhoofu kwa homa kwa muda wa siku 3–8.
- Uvimbe kwenye miguu na midomo ikiambatana na kutoka mate mengi.
- Mnyama hukosa uwezo wa kula kutokana na kuvimba midomo.
- Kupunguza uzalishaji wa maziwa.

### Tiba:

- Hakuna tiba rasmi lakini inashauriwa kuchanja.
- Tibu magonjwa nyemelezi.
- Kudhibiti na kuzuia:
- Kupiga marufuku usafirishaji wa mifugo.

... zaidi Uk. 12. »»








# Homa ya mapafu ya ng'ombe (Contagious bovine pleuropneumonia – CBPP)

***Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe ni ugonjwa unaowapata ng'ombe na nyati maji ambapo sehemu inayoathirika zaidi ni mapafu. Ugonjwa huu hauambukizi nyati pori. Husababishwa na bakteria waitwao Mycoplasma mycoides subsp. mycoides. Ugonjwa huu umeenea katika nchi nyingi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na una athari kubwa ya kiuchumi katika uzalishaji wa mifugo.***

**Linus Prosper**




### Dalili za ugonjwa huu

Dalili zinaweza kutofautiana na mara nyingi husambaa polepole, na kufanya ugonjwa huu kuwa vigumu kutambua katika hatua zake za mwanzo.

### Katika hali ya papo hapo:

- Homa: Joto la juu la 40°C (104°F) au zaidi.
- Matatizo ya kupumua: Kupumua kwa shida au haraka, mara nyingi kwa kuguna unapotoa pumzi, na kikohozi kikavu kinachoumiza.
- Mkao: Mnyama husimama huku kichwa na shingo ikiwa imepanuliwa, nyuma ikiwa na upinde kidogo, na viwiko vya mkono vikigeuka ili kurahisisha kupumua.
- Kupoteza hamu ya kula, uchovu, kupungua kwa uzalishaji wa maziwa, na kutokwa na maji puani.

### Katika hali sugu:

- Wanyama wengi huonekana kupata nafuu lakini wakawa wabebaji wa muda mrefu wa ugonjwa.
- Homa ya mara kwa mara, kupungua uzito, na kutovumilia mazoezi.

### Kwa ndama:

- Ulemavu na viungo kuwa na maumivu na kuvimba ni kawaida zaidi kuliko matatizo ya kupumua kwa ndama walio chini ya umri wa miezi sita.

Namna Ugonjwa Unavyoambukiza

CBPP huenea hasa kupitia mguso wa moja kwa moja, wa karibu, na unaorudiwa kati ya mnyama aliyeambukizwa na mwenye afya. Bakteria hupitia kwenye matone yanayotoka kwa mnyama mgonjwa wakati wa kukohoa.

### Njia zingine za usambaaji wa ugonjwa

- **Hewa:** Chini ya hali nzuri ya unyevu na upepo, pathojeni wanaweza kusafiri kwa umbali wa hadi mita 200.
- **Ndama tumboni:** Ugonjwa unaweza kuambukizwa kwa ndama akiwa bado tumboni kupitia kwenye placenta.
- **Wanyama wabebaji:** Wanyama wanaoambukizwa mara kwa mara ambao wanaonekana kuwa na afya njema lakini wagonjwa ni changamoto kubwa kwa jitihada za kudhibiti, kwani wanaweza kubeba maambukizi kwa muda wa miaka miwili na kusambaza kwa wengine.
- **Kuchanganya makundi:** Kuchanganya ng'ombe kutoka kwenye makundi mbalimbali katika maeneo ya malisho ya pamoja, mabwawa ya maji, soko, na wakati wa usafirishaji huongeza kwa kiasi kikubwa hatari ya maambukizi.

### Kudhibiti na kuzuia

CBPP ni ugonjwa unaotambuliwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH), na mikakati ya udhibiti inatofautiana kulingana na hali ya eneo.




**Maeneo yasiyo ya kawaida:** Nchi ambazo hazina CBPP huzingatia kuzuia kutokea kwake kupitia udhibiti wa uagizaji, usalama mkali wa viumbe hai, na kuwa na mpango wa dharura wa kukomesha milipuko yoyote.

**Kutokomeza:** Kwa kuweka wanyama karantini na uchinjaji wa mifugo iliyoambukizwa na iliyoathiriwa, pamoja na fidia kamili kwa wamiliki.

Maeneo yenye majanga: Katika maeneo ambayo kutokomeza ugonjwa huu kumeshindikana, kama vile sehemu kubwa ya Afrika, udhibiti unategemea programu za chanjo.

**Chanjo:** Chanjo zilizopunguzwa (k.m., aina ya T1/44) hutumiwa kupunguza viwango vya maambukizi. Uwepo wa wingi wa mifugo ni muhimu kwa ufanisi wa chanjo.

Udhibiti wa kutembea: Kuzuia ng'ombe kutembea husaidia kupunguza kuenea kwa ugonjwa.

**Tiba:** Matumizi ya antibiotiki kutibu CBPP haipendekezwi katika jitihada za kudhibiti. Ingawa inaweza kuficha ishara za dalili, mara nyingi haiondoi kabisa bakteria, na hivyo kusababisha uwezekano wa kuunda wanyama wabebaji wenye afya lakini wagonjwa.

***Kwa maelezo zaidi wasiliana na Daktari wa Mifugo Linus Prosper kwa simu namba 0756 663 247.***

# Je, ungependa kupata Jarida la Mkulima Mbunifu?

***Jarida la Mkulima Mbunifu linachapishwa na kutolewa kwa vikundi vya wakulima bure. Ili kikundi chako kipokee jarida hili, basi jaza fomu hii:***

1. Jina la kikundi/taasisi: ..........................................................................................................................

2. Mahali ulipo: ........................................................................................................................................

3. Idadi ya wanakikundi: Wanaume ..................................................... Wanawake ......................................................

4. Jina la kiongozi: ....................................................................................................................................

5. Nambari ya simu (rununu): ..................................................................................................................

6. Anuani ya posta: ...................................................................................................................................

***ILANI: Tafadhali ambatanisha majina ya wanakikundi kwenye karatasi tofauti pamoja na namba zao za simu.***

***Tuma fomu uliojaza kwa: S.L.P 14402, Arusha, Tanzania Ujumbe Mfupi Pekee: 0717 266 007, 0762 333 876 Barua pepe: info@mkulimambunifu.org Tovuti: www.mkulimambunifu.org***

# Ni muhimu kufahamu magonjwa ya ng'ombe

*... kutoka Uk. 10.*

- Ng'ombe wasipolishwa kwenye mazingira salama ni rahisi kushambuliwa na magonjwa.
- Kuwapatia chanjo wanyama wote waliopo katika eneo husika kwa usimamizi wa mtaalamu wa mifugo.

### 4. Kifua kikuu

Huu ni ugonjwa wa kichimu wa mifugo na binadamu. Visababishi ni bakteria wa aina tatu ambao husababisha matezi ya mnyama kudhoofika, ingawaje huweza kushambulia maeneo yote ya mnyama.

### Dalili za ugonjwa:

- Uvimbe katika matezi ya mnyama.
- Dalili hubadilika kutegemeana na eneo la ugonjwa yaani koo, mapafu, matiti au utumbo.
- Mnyama huanza kukohoa mfululizo na kupoteza uzito.

### Kudhibiti na kuzuia:

- Hakuna kinga wala tiba ya kisayansi kwa sasa, wala chanjo.
- Ondoa wanyama walioathirika zizini.

### 5. Ugonjwa wa homa ya mapafu

Ugonjwa huu husababishwa na bakteria kutoka kwenye kohozi la ng'ombe aliyeathirika.

### Dalili:

- Joto kali, mnyama kuzibwa.
- Kupumua kwa tabu.
- Kukohoa mfululizo.

### 6. Ugonjwa wa ndorobo

Ugonjwa huu husababishwa na vimelea wanaopatikana kwenye damu ya wanyama walioathirika. Mbung'o hueneza vimelea kutoka kwa ng'ombe mmoja hadi mwingine.

### Dalili:

- Dalili hujitokeza siku 5–7 baada ya kuenezwa na mbung'o.
- Ng'ombe hupoteza nguvu, joto kali na hushindwa kula.
- Uvimbe kwenye tezi na mara nyingine kuharisha.

### Tiba na kuzuia:

- Kuna aina nyingi za dawa kwa ajili ya tiba kama vile Berenil, Ethidium, Novidium, na Samorin.
- Epuka kuchunga ng'ombe kwenye misitu yenye mbung'o au karibu na wanyama pori.
- Kuondoa masalia ya mbung'o.



Picha:IN



Haki zote zimehifadhiwa ©2025 *Mkulima Mbunifu*